

a kibali cha kusafirisha na kuuza nyama ya ng'ombe kimataifa

* Tani 2,000 za nyama zauzwa nje ya nchi kwa miezi minne *

Na Scolastica Msewa, Morogoro

KAIMU Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, amesema usafirishaji wa nyama ya ng'ombe kimataifa umeongezeka hadi kufikia tano 2,000 katika kipindi cha miezi minne.

Amesema hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara.

Michael aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa jamii ya wafugaji wa ng'ombe wa kisasa uliofanyika mjini Morogoro.

Alisema baada ya agizo la Rais Samia, timu ya wataalamu wa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilipitia upya tozo zote kwa pamoja, ambapo hivi sasa kibali cha kusafirisha na kuuza nyama ya ng'ombe kimataifa ni sh. 40,000 bila kujali thamani ya mzigo wa mfanyabiashara.

Alitaja tozo nyingine kuwa ni ya bodi ya nyama ambayo ilikuwa ukipeleka nyama nje ya nchi, unatozwa asilimia moja ya mzigo uliosafirisha.

"Kwa hiyo lengo letu ni kupata fedha nyingi za kigeni kutokana na mauzo katika masoko ya nje ya nchi, hivyo tulibaini kuweka tozo nyingi kulizuia biashara ya nyama ya ng'ombe nje ya nchi," alieleza.

Kwa mujibu wa Michael, kipindi cha mwaka jana taifa lilipeleka tani 1,700 za nyama katika mataifa mbalimbali, lakini baada ya kupunguza tozo kumekuwa na ongezeko la upelekaji nyama ya ng'ombe kwa kipindi kifupi hadi kufikia tani 2,000 kwa miezi minne.


Naye, Mkufunzi mstaafu wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), Profesa Martin Shem, aliiomba serikali kuwekeza ujuzi na utaalamu wa ufugaji wa ng'ombe kwa kundi la vijana ili kuimarisha ufugaji nchini.

Alifafanua kuwa kundi kubwa la wafugaji nchini ni watu wazima na wazee, hivyo bila ya kuwa na mkakati maalumu wa kuhamasisha ufugaji kwa vijana taifa litafikia kipindi linaweza kuagiza nyama na hata mayai kutoka nje ya nchi.

Profesa Shem alisema taifa limebarikiwa kuwa na maeneo makubwa ya malisho na ya kutosha kwa ufugaji, hivyo liwekeze nguvu kubwa katika kuwarithisha vijana ufugaji.

Mwenyekiti wa jamii ya wafugaji wa ng'ombe wa kisasa, Naweed Mulla, alisema lengo la mkutano huo ni kukutanisha wadau wa ufugaji wa ng'ombe kisasa na serikali kuzungumzia kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wafugaji.

"Kupitia mkutano huu wa wafugaji wa kubwa wa ng'ombe tutawasilisha changamoto zetu za wafugaji kwa pamoja kwa zinafanana," alisema.



Sekta ya uvuvi ZiwaTanganyika kuboreshwa



Na Mwandishi Wetu, Kigoma

UHURU UK 6

SERIKALI ya Mkoa wa Kigoma, imesema mawaziri kutoka nchi nne za Tanzania, Zambia, Congo na Burundi watakutana mkoani humo, ili kuweka mkakati wa pamoja wa kuboresha sekta ya uvuvi Ziwa Tanganyika.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Rashid Machata, aliyasema hayo jana mkoani humo, wakati wa uzinduzi wa warsha ya siku mbili ya wadau wa mradi wa FISH4ACP ya kutekeleza mpango wa mradi ambao unalenga kuboresha mnyororo wa thamani wa dagaa na mgebuka katika Ziwa Tanganyika.

Mradi huo unatekelezwa na Shirika la Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na washirika kwa Ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) na Wizara ya Ushirikiano na Kiuchumi na Maendeleo ya Shirikishi la Ujerumani.

"Samaki wanakwenda Zambia, Congo na Burundi, hivyo nina taarifa hivi karibuni mawaziri kutoka nchi nne wa sekta ya uvuvi,

watakutana hapa Kigoma kuweka mikakati ya pamoja kusimamia uvuvi Ziwa Tanganyika," alisema.

Machata alisisitiza kuwa mradi wa FISH4ACP utekelezaji wake utafungua fursa za kiuchumi mkoani hapo.

Akifungua warsha hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), Dk. Rashid Tamatama, alisema serikali imeweka uzito mkubwa katika kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinavunwa kwa uendeleu katika maji yote nchini, yakiwemo ya Ziwa Tanganyika.

Dk. Tamatama alisema uvuvi endelevu na usimamizi makini wa rasilimali za uvuvi, unategemea kwa kiwango kikubwa uwepo wa taarifa nyingi sahihi za uvuvi na mtawanyo wa rasilimazi husika na zinazopatikana kwa wakati.

Katika kutatua changamoto sekta ya uvuvi, Dk. Tamatama alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imekuwa ikiweka juhudi

katika kutatua changamoto za wadau wa sekta ya uvuvi ili kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa nchi.

"Tunaboresha mazingira ya kufanya biashara za mazao ya uvuvi, kuzuia uvuvi haribifu, kuzuia utoroshwaji holela wa rasilimali za uvuvi na kuwezesha uvuvi endelevu," alisema.

Aliongeza kuwa: "Wizara kwa nyakati mbalimbali imeboresha kanuni za uvuvi na kufanya mapitio ya tozo ili kuzipunguza na kupunguza gharama za uendeshaji kwa wadau ili wahimili ushindani wa biashara ndani na nje ya nchi," alisema.

Mradi wa FISH4ACP ni Mpango wa Umoja wa Mataifa ya Afrika, Karibiani na Pasifiki unaochangia usalama wa chakula na lishe ustawi wa kiuchumi na uzalishaji wa ajira.

Mradi huo ulizinduliwa nchini mwanzoni mwa mwaka huu, ambapo utekelezaji wake unategemewa kuanza mwaka 2022 hadi 2024.





HABARI LEO UK 18.

Serikali kuendelea na uwekezaji sekta ya uvuvi

**Na Fadhili Abdallah,
Kigoma**

SERIKALI imesema uwekezaji kati-ka viwanda vya kuchakata samaki na uvuvi wa bahari kuu kutaiwezesha serikali kuongeza pato la taifa kupitia mazao ya uvuvi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya

Mifugo na Uvuvi (anayes-hughulikia uvuvi), Rashidi Tamatama akifungua warsha ya siku moja ya kutengeneza mpango mka-kati wa kuongeza mnyororo wa thamani ya dagaa na samaki aina ya migebuga kutoka Ziwa Tanganyika unaotekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO).

Tamatama alisema

kwa sasa sekta ya uvuvi inachangia asilimia moja tu kwenye pato la Taifa ingawa zipo fursa kubwa ya kuongeza pato hilo.

Alisema ni mpango wa serikali kuhakikisha uvuvi unafanyika kwenye bahari kuu ambao utaenda sambamba na ununuzi wa meli nne kubwa za uvuvi wa bahari kuu.

Sambamba na hilo alise-ma kuwa serikali iko kwe-nye utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa bandari za uvuvi nchini na kwamba kufikia mwaka 2025 mambo makubwa na mageuzi ya maendeleo yatakua yame-anza kutekelezwa.

Awali akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya utafiti wa samaki

nchini (TAFIRI), Dk Ismael Kimirei alisema kuwa utafiti mkubwa unatarajia kufanyika ili kujua kiwango cha rasilimali za uvuvi (samaki na dagaa) waliopo kwenye Bahari ya Hindi na maziwa makuu ya Tanzania ili kuweka mkakati wa uvu-naji na namna ya kuifanya sekta ya uvuvi kuwa na mchango mkubwa kwenye pato la taifa.

cy (DANIDA).
The research under the title
'Informal Sector and Social Pro-

of the research findings to differ-
ent stakeholders in Dar es Salaam
over the weekend.

the government must ensure ap-
propriate benefit packages, create
comprehensible information and
establish convenient enrolment

adding that the health and safety
policy should also be reviewed to
address issues of concerns afflict-
ing informal workers working in

DAILY NEWS Page 2.

Muleba authorities seize illegal fishing gears worth 12.5m/-

From MEDDY MULISA in Bukoba

AUTHORITIES in Muleba District have impounded various illegal fishing gear worth 12.5m/- and arrested 28 suspects in connection to the crime for further investigations, it has been disclosed.

Muleba District Commissioner (DC), Toba Nguvula, explained that the illegal fishing gear were impounded during an operation mounted by wananchi at Rulanda and Kimwani fishing camps.

"People have been sensitized to understand that Lake Victoria resources belong to them. Residents in villages surrounding Lake Victoria have mounted surveillance leading to the seizure of the fishing gear, including undersized nets and the 28 suspects," he said.

A few weeks ago, authorities in Muleba district impounded a consignment of Nile Perch fish that was being smuggled.

Mr Nguvula explained that the consignment was impounded at Luhanga fish landing site in Kikukwe Ward.

"Initial investigations revealed that the fish consignment was being transport-

ed on Lake Victoria to Karagwe District. Several suspects were helping in police investigations and they will be arraigned in court when investigations are completed," he said.

He explained that surveillance teams were on the alert to ensure that the government does not lose revenue due to smuggling.

Deputy Minister for Works and Transport, Mwita Waitara, recently toured Kagera region where he announced that the government is in the process to legalise a total of 693 unofficial ports in the country in a bid to improve marine transport, curb narcotic drugs and unlicensed firearms.

He explained that the strategy is also meant to facilitate movement of goods and services besides increasing revenue collections. A total of 348 of the 693 unofficial ports, almost 50 per cent, are on Lake Victoria which is surrounded by Kagera, Mwanza, Simiyu, Geita and Mara regions.

He revealed that at least 24 unofficial ports will be formalized during this financial year. He directed the Tanzania

Ports Authority (TPA) to revisit all levies charged at various ports to enable the government to come up with realistic charges.

The East African Community has designated the Lake Victoria basin as an 'economic growth zone', with the potential to develop into a major economic region.

The fisheries are vital in creating employment opportunities, mostly rural-based, thereby helping to reduce rural-urban migration. Fish is also a rich source of animal protein for human consumption and provides raw material (fishmeal) for processing animal feeds.

The fish industry contributes to GDP and has continued to be an important source of foreign exchange earned from fish exports. Besides, the fish industry contributes to the national and local government revenues through levying of various taxes, levies and license fees.

The sector has also contributed directly and indirectly to the improvement of physical infrastructure and social facilities, such as roads, schools and hospitals, particularly in remote fishing communities.